

Utendeza Unavyoathiri Urefu wa Irabu katika Kiswahili Sanifu

Pius Kiraka
Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Dodoma

piokiraka@yahoo.com

Ikisiri

Makala hii inachunguza namna viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, vinavyoathiri urefu wa irabu za neno pindi vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya Kiswahili Sanifu (KS). Data za utafiti huu zilikusanywa maktabani katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), kwa mbinu ya upitiaji nyaraka; na uwandani, huko Mji Mkongwe, Zanzibar, kupitia usaili. Data zilikuwa vidahizo vya KS vyenye uambishaji nyambulishi ambavyo vilitamkwa na wazungumzaji wa KS, kurekodiwa kwenye kinasa sauti, na kuchakatwa kwa programu ya kompyuta ili kubainisha nyakaa za irabu zinazotokea kwenye matamshi hayo. Uchanganuzi wa data uliongozwa na kiunzi cha dhana ya urefu, urefushaji, na ufupishaji kama zinavyotumiwa katika fani ya fonolojia na fonetiki. Matokeo ya uchanganuzi huo yanaonesha kuwa viambishi {-z-, -ez-, -iz-} vinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya KS, urefu wa irabu za maumbo mapya ya vitenzi unaweza: (i) kutobadilika katika irabu yoyote; au (ii) kubadilika kwa kurefushwa kwa irabu fulani, hasa inayotokea kabla ya kiambishi tamati hicho, inayopakana nacho; au (iii) kubadilika kwa kufupishwa kwa irabu ndefu iliyopo kwenye umbo la utenda. Aidha, makala inaonesha kuwa vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu za chini, <-aa>, vinaweza kutofautiana sana na vitenzi vingine vya K.S. pindi vinapoambatishiwa viambishi-tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, au viambishi vinginevyo.

Dhana za msingi: uambishaji nyambulishi, utendeza, urefu, urefushaji, ufupishaji

Utangulizi

Kwa miongo mingi, baadhi ya wanaisimu wa Kiswahili walikuwa na maoni kwamba kuna uwezekano wa lugha hii kuwa na irabu ndefu kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu (Ashton, 1977; Choge, 2009; Kimizi, 2003; Maganga, 1991; Massamba na wenzie, 2004; Polomé, 1967; Steere, 1943). Utafiti wa Kiraka (2013) ulithibitisha ukweli wa maoni hayo.

Kiraka (2013) alienda mbali kwa kubainisha mambo yanayosababisha kutokea kwa irabu ndefu katika maneno ya KS, hususani yale yaliyoingizwa katika kamusi za lugha hii ili yatolewe maana, yaani, vidahizo. Katika utafiti huo, mambo yaliyotajwa kuwa husababisha irabu ndefu kutokea kwenye vidahizo vya KS ni: (i) irabu ndefu kutokea kwa asili tu; au kwa nasibu; (ii) kurefushwa kwa irabu fupi katika milolongo ya konsonanti na kiyeyusho au milolongo ya konsonanti halisi; (iii) kubadili lafudhi ya kutamkia baadhi ya maneno yaliyotoholewa kutoka lugha nyinginezo; au (iv) kuungana kwa irabu katika mipaka ya mofimu.

Hata hivyo, tunapochunguza baadhi ya maneno ya KS, tunaona dhahiri kuwapo kwa irabu zinazotamkwa kwa wakaa mrefu zisizotokana na mazingira yaliyotajwa katika utafiti huo wa Kiraka (2013). Matalani, katika lugha hii, kuna maneno ambayo yana irabu fupi katika mzizi, kama vile <suka, nyoa, jua, taka>, lakini mizizi hiyo hiyo ya maneno hayo inapoambatishiwa viambishi fulanifulani ili kuunda maneno mapya, irabu hizo fupi za mzizi wa neno hubadilika na kusikika zikiwa na wakaa mrefu, kama vile <msu:si, kinyo:zi, uju:zi, sita:ki>. Kinyume chake, baadhi ya

maneno yenye irabu ndefu katika mzizi, kama vile <da:nga:nya, tu:a>, yanapoambatishiwa viambishi fulanifulani ili kuunda maneno mapya, irabu hizo ndefu za mzizi wa neno – zote au baadhi tu – hubadilika na kusikika zikiwa na wakaa mfupi kama vile <da:nganyana, kituo>. Hali kadhalika, sababu za kubadilika kwa wakaa wa irabu hizo hazielekei kuwa zile zinazotajwa katika utafiti huo. Hali hii inadokeza kuwa michakato fulanifulani ya uambishaji inayofanywa kwenye mizizi au mashina ya maneno ya KS huweza kuathiri au kutoathiri wakaa wa irabu mbalimbali zinazotokea katika maneno hayo.

Kwa mantiki hiyo, utafiti ulifanywa ili kuchunguza namna uambishaji nyambulishi unavyoweza kuathiri nyakaa za irabu pindi viambishi vyake vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya KS. Mchakato mmojawapo uliochunguzwa katika utafiti huo ni ule wa uambishaji nyambulishi wa utendeshi. Unyambulishi wa utendeshi ni mchakato unaowakilishwa na maumbo mengi zaidi - au, tuseme, *alomofu* nyingi zaidi – ukilinganishwa na michakato mingine (Ashton, 1977). Miongoni mwa *alomofu* hizo, *alomofu* zenye sifa za kuvutia sana linapokuja suala la viambishi na nyakaa za irabu ni {-z-, -ez-, -iz-}, au, tuseme, utendeza, kama ambavyo baadhi ya wanaisimu hupenda kuyarejelea maumbo haya katika miktadha isiyo rasmi pale wanapolenga kuyatofautisha na maumbo mengine yanayowakilisha mofimu ya utendeshi. Hivyo basi, makala hii inajadili namna viambishi tamati vya utendeza vinavyoathiri urefu wa irabu pindi vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya KS ili kuunda vitenzi vingine.

Kiunzi cha dhana

Data za utafiti uliochimbua makala hii zilichanganuliwa kwa kuongozwa na kiunzi kinachoundwa na dhana ya *urefu*, *urefushaji* na *ufupishaji* kama zinaavyotumiwa katika fani ya fonolojia na fonetiki. Kuhusu dhana ya *urefu*, Crystal (2008) anasema kuwa *urefu* ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya fonetiki kurejelea wakaa wa sauti au kitamkwa, na katika fonolojia hurejelea nyakaa za sauti na silabi pindi zinaposababisha tofauti kiisimu. Hali kadhalika, Trask (1996) anasema kuwa dhana ya *urefu* hurejelea wakaa wa kutamkwa kwa silabi, au irabu, au irabu-unganifu, ambao huchukuliwa kuwa ni sifa ya kifonolojia. Trask anaendelea kwa kusema kuwa dhana ya *urefu* ni sifa ya kifonolojia inayojitokeza katika lugha fulanifulani inayotofautisha vipandesauti vinavyofanana kupitia kiasi cha muda unaotumika katika kuvitamka. Matalani, anabainisha kuwa dhana ya *urefu* hutumiwa na lugha ya Kiitaliano kutofautisha maana ya neno /nono/ ‘tisa’ na /no:no/ ‘babu’; lugha ya Kiswidi huitumia kutofautisha maana ya neno /je:t/ ‘mbuzi’ na /jet:/ ‘-liopewa’; nayo lugha ya Kifini huitumia kutofautisha maana ya neno /kisa/ ‘mchezo’ na /kis:a/ ‘paka’. Naye Kiraka (2013) alibainisha kuwa lugha ya KS hutumia dhana ya *urefu* kutofautisha maana za maneno kama vile <kaka> ‘ganda tupu la yai’ na <ka:ka> ‘ndugu wa kiume’; <meza> ‘fanya kitu kumea’ na <me:za> ‘kifaa cha mbao’; <sita> ‘tarakimu iliyo kati ya tano na saba’ na <si:ta> ‘acha kutenda jambo baada ya kuonesha nia ya kutenda au baada ya kulianza’; <choma> ‘ingiza kitu chenye ncha ndani ya ngozi au nyama au kitu laini’ na <cho:ma> ‘unguza kwa moto’; na <tupa> ‘rusha kitu kwenda mbali’ na <tu:pa> ‘kifaa cha chuma cha kunolea vitu vingine’.

Utafiti huu ulichunguza dhana ya *urefu* katika vipandesauti vya irabu kwenye baadhi ya mashina ya vitenzi vya KS, kabla na baada ya maumbo yake ya utenda kuambatishiwa viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}. Hivyo basi, dhana ya *urefu* katika irabu ilimaanisha wakaa wa kusikika kwa irabu fulani, ambayo inaweza kuwa fupi au ndefu (Massamba, 2005).

Dhana nyingine iliyoongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ni *urefushaji*. Kwa mujibu wa Trask (1996), *urefushaji* ni mchakato wowote ambao, kifonetiki au kifonolojia, huongeza wakaa wa kipandesauti, nacho, mara nyingi, huwa ni irabu. Katika utafiti huu, dhana ya *urefushaji* ilichunguzwa kwenye baadhi ya mashina ya vitenzi vya KS ambavyo maumbo yake ya utenda huruhusu kuambatishiwa viambishi tamati, {-z-, -ez-, -iz-}, ili kuunda mashina ya vitenzi vya utendeza. Hivyo basi, dhana ya *urefushaji irabu* ilimaanisha mchakato unaoongeza wakaa wa irabu fulani fupi kwenye mashina hayo. Au, kama asemavyo Massamba (2005), *urefushaji irabu* ni mchakato wa kuifanya irabu, ambayo hapo awali ilikuwa fupi, kuwa ndefu.

Nayo dhana ya tatu iliyoongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ni *ufupishaji*. Trask (1996) anasema kuwa *ufupishaji* ni mchakato wowote wa kifonolojia unaosababisha kipandesauti kirefu kupoteza urefu wake. Mathalani, anadai, kwa nyakati mbalimbali, irabu ndefu za Kiingereza cha Kale zilifupishwa zilipotokea kabla ya milolongo fulanifulani ya konsonanti na katika silabi ya tatu kutoka mwisho wa neno, kama vile: *gōd-spell* > *god-spell* 'gospel' ('injili'), *cēpte* > *cepte* 'kept' ('-liotunzwa'), *Hlāf-mæsse* > *Hlammæsse* 'Lammas' ('Misa ya Mikate'), *sūþerne* > *superne* 'southern' ('-a kusini'). Katika utafiti huu, dhana ya *ufupishaji* ilichunguzwa kwenye baadhi ya mashina ya vitenzi vya KS ambavyo maumbo yake ya utenda

huruhusu kuambatishiwa viambishi tamati {-z-, -ez-, -iz-} ili kuunda mashina ya vitenzi vya utendeza. Hivyo basi, dhana ya *ufupishaji irabu* ilimaanisha mchakato unaopunguza wakaa wa irabu fulani ndefu kwenye mashina hayo, au mchakato unaoifanya irabu yenye wakaa mrefu kuwa na wakaa mfupi, hata kama irabu hiyo hutokea katika mazingira yanayoruhusu urefushaji (Massamba, 2005).

Methodolojia

Utafiti huu ulikuwa wa kitaamuli. Mbinu za usampulishaji zilizotumiwa ili kupata sampuli iliyotoa data za utafiti huu ni usampulishaji sinasibu na usampulishaji nasibu. Usampulishaji sinasibu ulitumiwa ili kuteua sampuli ya matini za KS zilizotumiwa kupata maneno ya KS yenye uambishaji nyambulishi. Nao usampulishaji nasibu, hususani usampulishaji nasibu tabakishi, ulitumiwa ili kuteua sampuli ya watoa taarifa waliotumiwa kupata matamshi ya maneno hayo.

Data za utafiti zilikusanywa maktabani na uwandani. Maktabani, katika Chuo Kikuu cha Dodoma, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka, kutoka kwenye sampuli isiyo nasibu, iliyoundwa na matini tatu ambazo ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (BAKITA, 2017), *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (BAKIZA, 2015), na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2014). Nako uwandani, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili kutoka kwenye sampuli nasibu iliyoundwa na wazungumzaji sita wa lugha ya KS kutoka Shehia ya Malindi na Shehia ya Shangani, katika eneo la Mji Mkongwe, Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar. Wazungumzaji hao walitakiwa kuwa na sifa mbalimbali zinazoendana na utafiti wa aina hii. Sifa mojawapo ilikuwa kujua kusoma maneno ya lugha hii yaliyoandikwa kwa kutumia alfabeti iliyowekwa na Kamati ya Usanifishaji. Sifa zao

nyingine zilizozingatiwa zilikuwa zile zilizopendekezwa na Batibo (1982), nazo ni watoa taarifa kuwa na umri usiopungua miaka 25 ili ujuzi wao wa lugha uwe umekwisha kukamilika; kutokuwa na athari ya lugha nyingine; kutokuwa na kasoro yoyote ya maumbile inayoweza kuleta tofauti katika matamshi, kama vile kutokuwa na baadhi ya meno; kutokuwa na matatizo yoyote katika matumizi yao ya lugha, kama vile kigugumizi, kithembe; kuelewa vizuri lugha inayotumiwa katika mawasiliano na mtafiti ili kueleza vipengele vya lugha; na watoa taarifa kuwa watu wenye muda mwingi wa kutosha kuweza kuvumilia maswali mengi na kuweza kujibu kikamilifu kama inavyotakiwa.

Data zilizokusanywa maktabani zilipelekwa uwandani. Data hizo zilikuwa orodha ya mashina ya vitenzi vya KS vyenye maumbo ya utenda yanayoruhusu kuambatishiwa viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, na orodha nyingine ya mashina hayo yakiwa yameambatishiwa viambishi tamati hivyo ili kuunda mashina ya vitenzi vya utendeza. Huko uwandani, vidahizo hivyo vilitamkwa na wazungumzaji wa KS. Matamshi hayo yalirekodiwa kwenye kinasasauti na kuchakatwa maabarani kwa kutumia programu ya kompyuta iitwayo *Speech Analyzer*.

Kwa kawaida, matamshi ya maneno hupakiwa kwenye programu hii, nayo programu huzalisha vielelezo vya kifonetiki vya matamshi hayo – au spektogramu – ambavyo hubainisha taarifa mbalimbali za kifonetiki kuhusu sauti hizo, kama vile umbo la mawimbi ya sauti, wakaa uliotumiwa kutamka vipashio mbalimbali vinavyounda sauti hizo, na kiwango cha kidatu, unguvunguvu. Matamshi ya wazungumzaji wa KS yalipakiwa kwenye programu hii na kuchakatwa ili kuchunguza nyakaa za irabu mbalimbali zinazotokea katika matamshi hayo. Mwishowe, data hizo

chakate zilichanganuliwa kwa kuongozwa na kiunzi cha dhana ya *urefu*, *urefushaji* na *ufupishaji* kama zinavyotumiwa katika fani ya fonolojia na fonetiki ili kueleza matokeo ya utafiti huu uliolenga kuchunguza namna uambishaji wa utendeza unavyoathiri urefu wa irabu katika vidahizo vya KS.

Matokeo ya utafiti

Wazungumzaji wa KS walipotamka mashina ya vitenzi vya lugha hii vyenye maumbo ya utenda na utendeza, kisha matamshi hayo yakapakiwa kwenye programu ya kompyuta ili kubainisha nyakaa za irabu mbalimbali zinazotokea kwenye maneno hayo, uchunguzi ulionesha kuwa irabu hizo zinaweza kuwekwa kwenye makundi mawili. Kundi la kwanza lina irabu ambazo hutamkwa kwa wakaa (au muda) wa wastani wa sekunde 0.1 katika usemaji wa kawaida wa lugha hii. Nalo kundi la pili lina irabu ambazo hutamkwa kwa wakaa wa wastani wa sekunde 0.2 katika usemaji wa kawaida wa lugha hii. Kwa sababu hiyo, irabu zilizotamkwa kwa wakaa mfupi (wastani wa sekunde 0.1) zilichukuliwa kuwa ni *irabu fupi* au *irabu zilizofupishwa*, nazo irabu zilizotamkwa kwa wakaa mrefu (wastani wa sekunde 0.2) zilichukuliwa kuwa ni *irabu ndefu* au *irabu zilizorefushwa*.

Baada ya kubainisha makundi haya mawili ya irabu za KS kutokana na nyakaa zake, utafiti huu ulichunguza nyakaa za irabu mbalimbali kwenye vitenzi vya lugha hii vyenye mashina ya utenda ili kujua kama nyakaa hizo ni fupi au ndefu. Kwa vile kanuni za kisarufi za KS huruhusu viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, kuambatishwa kwenye mashina haya ya utenda ili kuunda mashina mengine ya vitenzi vya lugha hii, yaani mashina ya vitenzi vya utendeza, basi utafiti huu ulichunguza pia nyakaa za irabu zilizopo kwenye mashina ya vitenzi vya utendeza ili kubainisha kama

wakaa wa irabu fulani unaweza kubadilika pindi kiambishi tamati cha utendeza kinapoambatishwa kwenye shina la utenda la kitenzi fulani cha lugha hii.

Utafiti unaonesha kuwa viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya KS vyenye maumbo ya utenda, viambishi hivyo huathiri urefu wa irabu za mashina hayo kulingana na aina ya silabi ishilizi iliyopo kwenye shina la utenda la kitenzi husika. Silabi hizo huwa na: (i) muundo wa konsonanti-irabu; au (ii) mkururo wa irabu mbili zinazotokea kwenye silabi mbili tofauti.

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na konsonanti-irabu

Baadhi ya vitenzi vya KS vinavyoishia na silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu katika umbo la utenda huruhusu kuambatishiwa viambishi tamati vya utendeza, {-ez-, -iz-}. Baadhi ya vitenzi hivyo vina irabu fupi tu zinazotokea kwa asili kwenye maumbo hayo ya utenda, ilhali vitenzi vingine vina mchanganyiko wa irabu fupi na irabu ndefu. Jedwali Na. 1 linaonesha baadhi ya vitenzi vyenye irabu fupi tu vinapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza.

Jedwali Na. 1: Vitenzi vya KS vinavyoishia na konsonanti-irabu, vyenye irabu fupi tu, vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<kata>	→	<kat + iz + a>	→	<katiza>
(ii)	<tata>	→	<tat + iz + a>	→	<tatiza>
(iii)	<sakama>	→	<sakam + iz + a>	→	<sakamiza>
(iv)	<iga>	→	<ig + iz + a>	→	<igiza>
(v)	<lipa>	→	<lip + iz + a>	→	<lipiza>

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(vi)	<shika>	→	<shik + iz + a>	→	<shikiza>
(vii)	<finya>	→	<finy + iz + a>	→	<finyiza>
(viii)	<inika>	→	<inik + iz + a>	→	<inikiza>
(ix)	<isha>	→	<ish + iz + a>	→	<ishiza>
(x)	<funika>	→	<funik + iz + a>	→	<funikiza>
(xi)	<uma>	→	<um + iz + a>	→	<umiza>
(xii)	<sukuma>	→	<sukum + iz + a>	→	<sukumiza>
(xiii)	<parura>	→	<parur + iz + a>	→	<paruriza>
(xiv)	<penya>	→	<peny + ez + a>	→	<penyeza>
(xv)	<kema>	→	<kem + ez + a>	→	<kemeza>
(xvi)	<okota>	→	<okot + ez + a>	→	<okoteza>
(xvii)	<gona>	→	<gon + ez + a>	→	<goneza>
(xviii)	<nong'ona>	→	<nong'on + ez + a>	→	<nong'oneza>

Chanzo: Utafiti (2023)

Tunapochunguza kwa makini matamshi ya maumbo ya utenda ya vitenzi vyote vilivyoorodheshwa kwenye Jedwali Na. 1, tunaona kuwa vitenzi hivyo vina irabu fupi tu. Kiambishi tamati cha utendeza, {-iz-} au {-ez-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi hivyo ili kuunda vitenzi vingine, maumbo ya vitenzi vipya vinavyozaliwa nayo husikika yakiwa na irabu fupi tu. Hivyo basi, uambishaji wa utendeza hauathiri nyakaa za irabu katika vitenzi vya kundi hili.

Vitenzi vingine vya KS vinavyoishia na silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu vinaweza kuwa na mchanganyiko wa irabu fupi pamoja na irabu ndefu kwenye maumbo yake ya utenda. Baadhi ya vitenzi hivyo vinaweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza ili kuunda vitenzi vingine, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 2 linalofuata.

Jedwali Na. 2: Vitenzi vya KS vinavyoishia na konsonanti-irabu, vyenye irabu fupi na ndefu, vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<de:ka>	→	<de:k + ez + a>	→	<de:keza>
(ii)	<ko:sha>	→	<ko:sh + ez + a>	→	<ko:sheza>
(iii)	<to:sha>	→	<to:sh + ez + a>	→	<to:sheza>
(iv)	<go:mba>	→	<go:mb + ez + a>	→	<go:mbeza>
(v)	<pe:nda>	→	<pe:nd + ez + a>	→	<pe:ndeza>
(vi)	<te:ndeka>	→	<te:ndek + ez + a>	→	<te:ndekeza>
(vii)	<da:ka>	→	<da:k + iz + a>	→	<da:kiza>
(viii)	<fa:nya>	→	<fa:ny + iz + a>	→	<fa:nyiza>
(ix)	<fi:sha>	→	<fi:sh + iz + a>	→	<fi:shiza>
(x)	<li:mbika>	→	<li:mbik + iz + a>	→	<li:mbikiza>
(xi)	<ba:ndika>	→	<ba:ndik + iz + a>	→	<ba:ndikiza>
(xii)	<ga:ndama>	→	<ga:ndam + iz + a>	→	<ga:ndamiza>
(xiii)	<i:njika>	→	<i:njik + iz + a>	→	<i:njikiza>
(xiv)	<fu:ngama>	→	<fu:ngam + iz + a>	→	<fu:ngamiza>
(xv)	<fu:ka>	→	<fu:k + iz + a>	→	<fukiza>

Chanzo: Utafiti (2023)

Vitenzi vilivyoorodheshwa katika Jedwali Na. 2 vinajumuisha irabu fupi pamoja na irabu ndefu kwenye maumbo yake ya utenda. Tukichunguza matamshi ya wazungumzaji wa KS, tunaona kuwa pindi kiambishi tamati cha utendeza, {-ez-} au {-iz-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi hivyo ili kuunda vitenzi vingine, umbo jipya linalozaliwa nalo huendelea kuwa na irabu fupi pamoja na irabu ndefu katika nafasi zilezile zinamotokea kwenye umbo la utenda (taz. Mifano Na. (i)-(xiv)). Kwa mantiki hiyo, uambishaji wa utendeza hauathiri urefu wa irabu yoyote katika vitenzi hivyo.

Kwa upande mwingine, tunapochunguza matamshi ya umbo la utenda la kitenzi cha mwisho katika orodha hiyo, <fu:ka> (taz. Mfano Na. 15), tunaona kuwa kuna irabu ndefu inayotokea kwenye silabi ya kwanza. Hata hivyo, pindi kiambishi tamati cha utendeza kinapoambatishwa kwenye shina hilo ili kuunda kitenzi kingine, <fukiza>, irabu hiyo ndefu kwenye silabi ya kwanza hufupishwa, na kufanya irabu zote zilizopo kwenye umbo jipya kusikika zikiwa fupi. Kwa sababu hiyo, uambishaji wa utendeza huathiri wakaa wa irabu katika kitenzi hiki kwa kufupisha irabu ndefu ya mzizi wa kitenzi hicho. Vipengele vinavyofuata vinatalii vitenzi vingine vinavyoishia na silabi zisizokuwa na muundo wa konsonanti-irabu.

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na milolongo ya irabu

Ukiacha vitenzi vinavyoishia na silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu, vitenzi vingine vya KS vinavyoweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza ili kuunda vitenzi vingine ni vitenzi vinavyoishia na milolongo ya irabu. Kuna makundi matano ya vitenzi hivyo katika lugha hii, nayo ni yale yanayoishia na milolongo <-ea>, <-ia>, <-oa>, <-ua>, na <-aa>. Wakati vitenzi vya lugha hii vinavyoishia na silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu huweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza cha {-ez-} au cha {-iz-} kwenye mashina ya utenda, vitenzi vinavyoishia na milolongo ya irabu huruhusu kuambatishiwa umbo lilelile moja tu la kiambishi tamati cha utendeza, nalo ni {-z-}.

Athari za utendeza kwa urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo <-ea>

Kama tulivyoona kwenye vitenzi vya KS vinavyoishia na silabi yenye muundo wa konsonanti-irabu, baadhi ya vitenzi vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-ea> navyo vinaweza kuwa na irabu fupi tu, huku vitenzi vingine

vikiwa na mchanganyiko wa irabu fupi pamoja na irabu ndefu. Jedwali Na. 3 linaonesha baadhi ya vitenzi vya lugha hii vinavyoishia na mlolongo huo pindi vinapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza {-z-}.

Jedwali Na. 3: Vitenzi vya KS vinavyoishia na <ea> vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda →	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi →	Umbo la utendeza →
(i)	<to:kea> →	<to:ke + z + a> →	<to:keza>
(ii)	<e:ndelea> →	<e:nde + z + a> →	<e:ndeza>
(iii)	<go:ngomea> →	<go:ngome + z + a> →	<go:ngomeza>
(iv)	<ko:ngomea> →	<ko:ngome + z + a> →	<ko:ngomeza>
(v)	<jo:ngea> →	<jo:nge + z + a> →	<jo:ngeza>
(vi)	<kwe:a> →	<kwe: + z + a> →	<kwe:za>
(vii)	<te:mbea> →	<te:mbe + z + a> →	<te:mbeza>
(viii)	<elea> →	<ele + z + a> →	<eleza>
(ix)	<enea> →	<ene + z + a> →	<eneza>
(x)	<legea> →	<lege + z + a> →	<legeza>
(xi)	<teketea> →	<tekete + z + a> →	<teketeza>
(xii)	<bonyea> →	<bonye + z + a> →	<bonyeza>
(xiii)	<kolea> →	<kole + z + a> →	<koleza>
(xiv)	<sogea> →	<soge + z + a> →	<sogeza>
(xv)	<zoea> →	<zoe + z + a> →	<zoeza>
(xvi)	<pe:mbea> →	<pe:mbe + z + a> →	<pe:mbe:za>
(xvii)	<te:ngea> →	<te:nge + z + a> →	<te:nge:za>
(xviii)	<potea> →	<pote + z + a> →	<pote:za>

Chanzo: Utafiti (2023)

Katika Jedwali Na. 3, tunaona kuwa baadhi ya vitenzi vya KS vyenye irabu fupi na irabu ndefu (taz. Mifano Na. 3 (i)- (vii) vinapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, kwenye mashina yake ya utenda ili kuunda vitenzi vingine, irabu zake ndefu huendelea kusikika kuwa ni ndefu, nazo irabu fupi huendelea kusikika kuwa ni fupi kwenye umbo la kitenzi kipya kinachozaliwa. Aidha, baadhi ya vitenzi vya lugha hii vina irabu fupi

tu (taz. (viii) - (xv)), navyo vinapoambatishiwa kiambishi tamati hicho, huendelea kusikika vikiwa na irabu fupi tu kwenye umbo jipya linalotokea. Kwa upande mwingine, kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya baadhi ya vitenzi vya KS, kinaweza kurefusha irabu fupi inayotokea kabla ya kiambishi tamati hicho, inayopakana nacho (taz. (xvi) - (xviii)).

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo <-ia>

Vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-ia> kwenye umbo la utenda vinaweza kuwa ama na irabu fupi tu au mchanganyiko wa irabu fupi na irabu ndefu. Maumbo hayo yanaweza pia kunyambuliwa kwa kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, ili kuunda vitenzi vingine. Tazama Jedwali Na. 4 linalofuata.

Jedwali Na. 4: Vitenzi vya K.S. vinavyoishia na <-ia> vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<chu:kia>	→	<chu:ki + z + a>	→	<chu:kiza>
(ii)	<tu:kia>	→	<tu:ki + z + a>	→	<tu:kiza>
(iii)	<vi:a>	→	<vi: + z + a>	→	<vi:za>
(iv)	<i:ngia>	→	<i:ngi + z + a>	→	<i:ngiza>
(v)	<a:ngalia>	→	<a:ngali + z + a>	→	<a:ngaliza>
(vi)	<a:ngamia>	→	<a:ngami + z + a>	→	<a:ngamiza>
(vii)	<ki:mbia>	→	<ki:mbi + z + a>	→	<ki:mbiza>
(viii)	<ta:ngulia>	→	<ta:nguli + z + a>	→	<ta:nguliza>
(ix)	<tu:mbukia>	→	<tu:mbuki + z + a>	→	<tu:mbukiza>
(x)	<didimia>	→	<didimi + z + a>	→	<didimiza>
(xi)	<bugia>	→	<bugi + z + a>	→	<bugiza>
(xii)	<kawia>	→	<kawi + z + a>	→	<kawiza>
(xiii)	<umia>	→	<umi + z + a>	→	<umiza>
(xiv)	<lia>	→	<li + z + a>	→	<liza>

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(xv)	<ning'inia>	→	<ning'ini + z + a>	→	<ning'iniza>
(xvi)	<nua>	→	<nui + z + a>	→	<nuiza>
(xvii)	<timia>	→	<timi + z + a>	→	<timiza>
(xviii)	<tulia>	→	<tuli + z + a>	→	<tuliza>
(xix)	<sikia>	→	<siki + z + a>	→	<siki:za>

Chanzo: Utafiti (2023)

Tunapochunguza matamshi ya wazungumzaji wa KS, tunaona kuwa kiambishi-tamati cha utendeza, {-z-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi yenye mchanganyiko wa irabu fupi na irabu ndefu (taz. Mifano Na. (i)-(ix)), irabu hizo huendelea kuwa na hali hiyohiyo katika maumbo mapya yanayotokea. Kwa vitenzi vilivyo na irabu fupi tu kwenye umbo la utenda (taz. (x)-(xviii)), kiambishi tamati cha utendeza kinapoambatishwa kwenye mashina hayo, kinaweza pia kisiathiri urefu wa irabu yoyote kwenye umbo jipya linalozaliwa, au kinaweza kurefusha irabu inayotokea kabla ya kiambishi tamati cha utendeza, inayopakana nacho (taz. (xix)).

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo <-oa>

Kundi lingine ni lile la vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-oa>. Maumbo ya utenda ya vitenzi vinavyoishia na mlolongo huo yanaweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, ili kuunda vitenzi vingine, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Vitenzi vya KS vinavyoishia na <-oa> vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<toa>	→	<to + z + a>	→	<toza>
(ii)	<kokotoa>	→	<kokoto + z + a>	→	<kokotoza>
(iii)	<chomoa>	→	<chomo + z + a>	→	<chomoza>
(iv)	<poa>	→	<po + z + a>	→	<po:za>
(v)	<kohoa>	→	<koho + z + a>	→	<koho:za>
(vi)	<dokoa>	→	<doko + z + a>	→	<doko:za>
(vii)	<oa>	→	<o + z + a>	→	<o:za>
(viii)	<kojoa>	→	<kojo + z + a>	→	<kojo:za>
(ix)	<komoa>	→	<komo + z + a>	→	<komo:za>

Chanzo: Utafiti (2023)

Matamshi ya wazungumzaji wa lugha hii yanaonesha kuwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-oa>, kinaweza kisiathiri urefu wa irabu zilizopo kwenye maumbo mapya yanayozaliwa (taz. (i)-(iii)). Irabu fupi huendelea kusikika zikiwa fupi.

Kwa upande mwingine, kuambatisha kiambishi tamati cha utendeza, {-z-} kwenye mashina ya utenda ya baadhi ya vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-oa> kunaweza kurefusha irabu fupi inayotokea kabla ya kiambishi tamati cha utendeza, inayopakana nacho (taz. (iv)-(ix)). Katika kipengele kinachofuata, tutachunguza vitenzi vya lugha hii vinavyoishia na mlolongo wa <-ua>.

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo <-ua>

Vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu wa <-ua> vinaweza kuwa na irabu fupi tu kwenye umbo la utenda, au kuwa na mchanganyiko

wa irabu fupi na irabu ndefu kwenye umbo hilo. Baadhi ya vitenzi hivyo vinaweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, ili kuunda vitenzi vingine. Tazama Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Vitenzi vya KS vinavyoishia na <-ua> vinapoambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<ugua>	→	<ugu + z + a>	→	<uguza>
(ii)	<chipua>	→	<chipu + z + a>	→	<chipuza>
(iii)	<chapua>	→	<chapu + z + a>	→	<chapuza>
(iv)	<jua>	→	<ju + z + a>	→	<juza>
(v)	<kua>	→	<ku + z + a>	→	<kuza>
(vi)	<parua>	→	<paru + z + a>	→	<paruza>
(vii)	<cha:gu>	→	<cha:gu + z + a>	→	<cha:guza>
(viii)	<u:ngua>	→	<u:ngu + z + a>	→	<u:nguza>
(ix)	<pu:ngua>	→	<pu:ngu + z + a>	→	<pu:nguza>
(x)	<ta:ngua>	→	<ta:ngu + z + a>	→	<ta:nguza>
(xi)	<ta:ndua>	→	<ta:ndu + z + a>	→	<ta:nduza>

Chanzo: Utafiti (2023)

Uchunguzi wa matamshi ya wazungumzaji wa KS unaonesha kuwa kiambishi-tamati cha utendeza, {-z-}, kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya lugha hii, hakiathiri urefu wa irabu zinazotokea kwenye maumbo mapya yanayozaliwa. Irabu fupi huendelea kuwa fupi (taz. (i) - (vi)), nazo irabu ndefu zikiendelea kusikika kuwa ndefu (taz. (vii) - (xi)).

Utendeza unavyoathiri urefu wa irabu za vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo <-aa>

Kundi la mwisho la vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo ya irabu vinavyoweza kuambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, ni lile lenye vitenzi vinavyoishia na mlolongo wa irabu-pacha za chini, <-aa>. Kama tulivyoona kwenye vitenzi vya makundi mengine, mashina ya utenda

ya baadhi ya vitenzi vya kundi hili nayo yanaweza kuwa na irabu fupi tu, au kuwa na mchanganyiko wa irabu fupi na irabu ndefu. Jedwali Na. 7 linaonesha baadhi ya vitenzi vya kundi hili ambavyo mashina yake yanaweza kuambatishiwa kiambishi-tamati cha utendeza, {-z-}.

Jedwali Na. 7: Vitenzi vya KS vinavyoishia na <-aa> vinapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza

Na.	Umbo la utenda	→	Mzizi + Kiambishi cha utendeza + Irabu ishilizi	→	Umbo la utendeza
(i)	<chakaa>	→	<chaka + z + a>	→	<chaka:za>
(ii)	<dumaa>	→	<duma + z + a>	→	<duma:za>
(iii)	<duwaa>	→	<duwa + z + a>	→	<duwa:za>
(iv)	<jaa>	→	<ja + z + a>	→	<ja:za>
(v)	<paa>	→	<pa + z + a>	→	<pa:za>
(vi)	<kataa>	→	<kata + z + a>	→	<kata:za>
(vii)	<komaa>	→	<koma + z + a>	→	<koma:za>
(viii)	<kunyaa>	→	<kunya + z + a>	→	<kunya:za>
(ix)	<lemaa>	→	<lema + z + a>	→	<lema:za>
(x)	<ng'aa>	→	<ng'a + z + a>	→	<ng'a:za>
(xi)	<nyamaa>	→	<nyama + z + a>	→	<nyama:za>
(xii)	<pakaa>	→	<paka + z + a>	→	<paka:za>
(xiii)	<shupaa>	→	<shupa + z + a>	→	<shupa:za>
(xiv)	<sinyaa>	→	<sinya + z + a>	→	<sinya:za>
(xv)	<tapakaa>	→	<tapaka + z + a>	→	<tapaka:za>
(xvi)	<kakamaa>	→	<kakama + z + a>	→	<kakama:za>
(xvii)	<zagaa>	→	<zaga + z + a>	→	<zaga:za>
(xviii)	<pagaa>	→	<paga + z + a>	→	<paga:za>
(xix)	<zubaa>	→	<zuba + z + a>	→	<zuba:za>
(xx)	<a:mbaa>	→	<a:mba + z + a>	→	<a:mba:za>
(xxi)	<a:ngaa>	→	<a:nga + z + a>	→	<a:nga:za>
(xxii)	<pu:mbaa>	→	<pu:mba + z + a>	→	<pu:mba:za>
(xxiii)	<sa:mbaa>	→	<sa:mba + z + a>	→	<sa:mba:za>
(xxiv)	<sha:ngaa>	→	<sha:nga + z + a>	→	<sha:nga:za>
(xxv)	<ta:mbaa>	→	<ta:mba + z + a>	→	<ta:mba:za>
(xxvi)	<ta:ndaa>	→	<ta:nda + z + a>	→	<ta:nda:za>
(xxvi)	<ta:ngaa>	→	<ta:nga + z + a>	→	<ta:nga:za>

Chanzo: Utafiti (2023)

Tofauti na vitenzi vya makundi mengine tuliyokwishayajadili, vitenzi vya lugha hii vinavyoishia na mlolongo wa irabu za chini, <-aa>, vinapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, ili kuunda vitenzi vingine, hurefusha irabu inayotokea kabla yake, inayopakana nacho, katika kila kitenzi kinachoambatishiwa kiambishi tamati hicho. Tumeona kuwa kiambishi tamati cha utendeza kinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya makundi mengine, si rahisi kutabiri iwapo uambatishaji huo utaathiri urefu wa irabu kwenye maumbo mapya ya vitenzi yatakayozaliwa. Hata hivyo, kwa vitenzi vinavyoishia na mlolongo wa irabu za chini, <-aa>, hali inaonekana kuwa tofauti kwa sababu matokeo ya uambatishaji huo yanatabirika, ambapo kila shina la kitenzi kinachoishia na mlolongo huo linapoambatishiwa kiambishi tamati cha utendeza, {-z-}, huzaa umbo jipya la kitenzi lililo na irabu iliyorefushwa, inayotokea kabla ya kiambishi-tamati hicho, na kupakana nacho.

Hili ni jambo la kustaajabisha. Kwa nini vitenzi vinavyoishia na irabu-pacha za chini, <-aa>, hutofautiana sana na vitenzi vingine vya lugha hii vinavyokubali kuambatishiwa kiambishi hicho? Hata hivyo, kama tutakavyoona katika utafiti wa Kiraka (2023), vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu za chini, <-aa>, vinaelekea kuwa na sifa za kuvutia sana, zinazotofautiana na za vitenzi vingine, pale mashina yake yanapoambatishiwa viambishi mbalimbali vya lugha hii. Kwa sababu hiyo, vitenzi hivyo vinapaswa kuchunguzwa kwa makini sana, pasipo kuvieleza jumlajumla tu pamoja na vitenzi vingine.

Hitimisho

Makala hii imewasilisha matokeo ya utafiti uliochunguza namna viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, vinavyoweza kuathiri urefu wa irabu pindi vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya KS vyenye maumbo ya utenda. Utafiti huo umeonesha kuwa viambishi tamati hivyo vinapoambatishwa kwenye mashina ya vitenzi vya lugha hii vyenye maumbo ya utenda, kuna hali za namna tatu zinazoweza kutokea kuhusu urefu wa irabu za maumbo mapya yanayozaliwa baada ya uambatishaji huo. Hali ya kwanza inayotokea pindi viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, vinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya KS ni kutobadilika kwa urefu wa irabu yoyote ya vitenzi vipya vinavyozaliwa. Irabu fupi zilizopo kwenye umbo la awali huendelea kuwa fupi, nazo irabu ndefu huendelea kuwa ndefu. Hali ya pili inayotokea pindi viambishi tamati hivyo vinapoambatishwa kwenye mashina ya utenda ya vitenzi vya lugha hii ni kurefushwa kwa irabu fulani katika umbo jipya la kitenzi linalozaliwa, hasa irabu inayotokea kabla ya kiambishi tamati hicho, na inayopakana nacho. Nayo hali ya tatu inayoweza kutokea pindi mashina ya utenda ya vitenzi vya lugha hii yanapoambatishiwa viambishi tamati vya utendeza ni kufupishwa kwa irabu ndefu iliyopo kwenye umbo la utenda na irabu hiyo kusikika ikiwa na wakaa mfupi kwenye umbo jipya la utendeza linalozaliwa.

Zaidi ya hayo, makala hii imeonesha kuwa vitenzi vya KS vinavyoishia na mlolongo wa irabu za chini, <-aa>, vinatofautiana na vitenzi vinavyoishia na vipashio vingine pale vinapoambatishiwa viambishi tamati vya utendeza, {-z-, -ez-, -iz-}, kwa sababu athari zake kwa urefu wa irabu za maumbo mapya yanayozaliwa zinaweza kutabirika, tofauti na vitenzi vingine.

Marejeleo

- Ashton, E. O. (1977). *Swahili Grammar (including intonation)* (3rd impression). London, UK: Longman Group Ltd.
- Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (chapa ya 3). Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers Limited.
- Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) (2015). *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (chapa ya pili). Nairobi, Kenya: Oxford University Press.
- Batibo, H. M. (1982). Mbinu za Kuchunguza na Kuainisha Fonimu katika lugha za Kiafrika. Katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) (Mh.), *Makala za semina za TUKI na makala mbalimbali za wachunguzi* (uk. 1 - 16). Dar es Salaam, Tanzania: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Choge, S. C. (2009). Understanding Kiswahili Vowels. *The Journal of Pan African Studies*, 2(8), 62 - 77.
- Crystal, D. (2008). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics* (6th ed.). Malden, MA: Blackwell Publishing.
- Kimizi, M. M. (2003). *The Syllable Structure in Standard Kiswahili* (Unpublished Master's Dissertation). University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Kiraka, P. (2013). *Urefu, Urefushaji na Ufupishaji wa Irabu katika Kiswahili Sanifu* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Kiraka, P. (2023). *Ruwaza za Urefu, Urefushaji na Ufupishaji wa Irabu katika Kiswahili Sanifu* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.
- Maganga, C. (1991). *A Study of the Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi* (Unpublished PhD

Thesis). University of Dar es Salaam, Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2005). The Role of ‘Suprasegmental’ Phenomena in the Analysis of Bantu Languages: With Special Reference to Ciruuri. *Occasional Papers in Linguistics*, 1, 88-105.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Polomé, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington D. C.: Center for Applied Linguistics.

Steere, E. (1943). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar* (4th ed.). London, UK: Society for Promoting Christian Knowledge.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la tatu). Nairobi, Kenya: Oxford University Press.

Trask, R. L. (1996). *A Dictionary of Phonetics and Phonology*. London, UK: Routledge.